# MAANA YA MAENDELEO NI NINI?

## MFANO WA MAFIA, TANZANIA

kwa Professor Patricia Caplan, BA, MA, Ph.D.
Goldsmiths College, University of London

Hotuba hii imetolewa tarehe 1I agosti 1994
Lizu Hotel, Kilindoni, Mafia

Imetayarishwa na Changia Maendeleo Mafia (Chamama)

Hotuba hii imetafisiriwa kwa msaada wa
Nd. Mikidadi Juma Kichange.

## MAANA YA MAENDELEO NI NINI? MFANO WA MAFIA

### DIBAJI

Naona nimepewa heshima kubwa kuweza kupata nafasi ya kuwahutubia watu wengi kama hivi wakiwa na nyadhifa tofauti, leo hii. Pamoja na kunipatia nafasi hii, mimi bado napata wasiwasi kidogo kuongelea maendeleo ya Mafia hasa mimi nikiwa si Mtanzania.

Isitoshe, watu wengi wa Mafia wameniita inara nyingi mimi mwenyeji. Nashukuru kwa heshima hiyo tukufu. Heshima hiyo, pia, imenifanya mpaka mimi nione Mafia kama mji wangu wa pili, ambao imejaa wazazi wangu, ndugu zangu, dada zangu, kaka zangu, akina babu na bibi zangu, na marafiki zangu. Miaka 29 iliyopita tangu nifike Mafia mwaka sitini na tano, nimeweza kujifunza mambo mengi, na watu wamekuwa tayari kunifundisha mambo mengi, lakini kila mara, naona bado yapo mengi ya kujifunza na kwamba nahitaji muda zaidi. Na huenda, kwa bahati mbaya, mengine sikuyajua vizuri, nadhani mtanisamehe. Nimeamua kuzungumza kwa Kiswahili na nadhani mtakubaliana nami kuwa Kiswahili changu si kizuri sana lakini mtakuwa radhi kunivumilia na kunisikiliza. Baada ya hayo, machache, naomba sasa tuingie katika maada maalum nitakayoizungumzia leo hii.

### MAANA YA MAENDELEO NI NINI ?

Sifikiri kama tunaweza kuyapima maendeleo kwa wingi wa mahoteli makubwa au kwa wingi wa vyupa vya masoda, au wingi wa magari waliyonayo matajiri. Maendeleo hasa maana yake ni kama yafuatavyo:

- Kwanza ni afya na ustawi wa jamii ya watu.
- Pili ni Elimu.
- Tatu ni mishahara inayofaa
- Nne kuinuka kwa hali ya maisha na upatikanaji rahisi wa mahitaji ya lazima.

Vipi tunaweza kupata maendeleo?

- Yatubidi tufikirie mambo muhimu ambayo tunaweza kuyatumia katika kuipata maendeleo, kwani kila kitu ni nyenzo ya maendeleo kwa pale pahali kilipo.
- Yatubidi kuheshimu na kutumia maumizi walionao watu wetu, kwani wao ndio wataalamu zaidi wa maeneo wanayotoka.
- Yatubidi kuwasikiliza wanayosema na kuzingatia wanayohitaji kwa maisha yao, ili kuwepo na urahisi wa kuweza kufanya katika mendeleo. Kwa kifupi maendeleo huanza chini, na hayawezi kuletwa kutoka juu. Hii haina maana ya kwamba katika maendeleo hakuhitajiki maelekezo kutoka juu, wataalamu kutoka nje, au ufundi kutoka mbali. Inawezekana lakini yatupasa tuwe waangalifu jinsi maendeleo haya yatakavyo saidia na jinsi yalivyokubalika, kwa wakati huo, mahali hapo kwa watu hao.

**MAENDELEO KWA AJILI YA NANI ?**

Katika nchi nyingi za Kusini au nchi za 'dunia ya tatu', unaweza kuona majengo makubwa katika miji, mabenki, viwanda, na mahoteli. India yaweza ikawa mfano mzuri. Lakini watu wa Barahindi wamebaki maskini, wanalima lakini bila ya kujitosheleza kwa chakula. Hii si maana halisi ya maendeleo, haya ni maendeleo ya baadhi na baadhi ya watu tu.

Tangu Tanzania ipate Uhuru, serikali imejitahidi kulikwepa tatizo lili, na nafikiri kuendelea kulikwepa maradufu. Vinginevyo, itajikuta imejenga nchi ya mataifa mawili, nchi moja kukaliwa na matajiri, na nchi nyingine kukaliwa na watu maskini sana.

**MAFIA**

Kila ninapokuja Mafia, watu huniuliza juu ya mabadiliko ya kimaendeleo ninayoyaona kama yapo. Wengi hakuna maendeleo tangu kupatikana uhuru. Mimi nasema si kweli, hata kidogo. Naomba nianze na upande wa kwamba yapo maendeleo. Kwanza hebu tujaribu kuona jambo la muhimu la kuangaliwa katika Tanzania tangu uhuru. Tanzania imefaidika kwa amani na utulivu kuliko sehemu nyingi za Afrika, hivi sasa. Hakuna migogoro ya kidini, hakuna migogoro ya makabila, hakuna vita vya wenyewe kwa wenyewe, hakuna vita kati ya Tanzania na nchi za jirani. Tukiangalia sehemu nyingine za Afrika, tutaona kuwa nchi ya Tanzania ni nchi ya bahati. Angalia Somalia, Angola, Mozambique, Liberia, Sudan, Burundi na Rwanda, nchi ambazo zinatukumbusha na kutufundisha kuwa amani ni baraka, na lazima itunzwe na kuheshimiwa

Hebu natuangalie mabadiliko yaliyokwishatokea kati ya miaka sitini na tisini.

***a) Elimu***

Nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza mwaka sitini na tano, Mafia kulikuwa na shule chache sana za msingi, na zilikuwa zinaishia darasa la nne tu. Ni vijana wachache waliokuwa wakienda kuendelea na masomo, walipelekwa kusoma bara. Hata hivyo, wengi wa vijana waliosoma wakati huo, walikuwa wavulana tu. Nilipokuja mara ya pili mwaka 1976 kulikuwa na mafanikio kidogo: watoto walikuwa wakienda shule, wakike na wakiume, na kulikuwa na ongezeko kubwa la shule za misingi, hadi darasa la saba. Kanga, kwa mfano, kulikuwa na darasa la sita kwa Kanga na Bweni la kufurahisha sasa ni kwamba kila kijiji kina shule yake hadi darasa la saba. Hali kadhalika, hivi sasa Mafia ina shule ya Sekondari. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wote wa Mafia waliojenga shule hii kwa pamoja. Kitendo hiki ni cha maendeleo makubwa.

***b) Afya***

Nilipokuja mwaka 1965 kulikuwa na zahanati chache vijijini na hospitali ndogo mjini Kilindoni. Wakati

huo, zahanati zilikuwa na watumishi wachache waliochukuwa mafunzo. Nilipokuja tena mwaka 1976, nilizikuta hospitali hizo na nyingine zilikuwa zimepewa wakunga, na kwa mwaka 1985 (safari yangu ya tatu) kulikuwa na MCH Clinic zinapelekwa kwa kila kituo cha afya wilayani. Hali hii ni bora sasa kuliko pale nyuma. Leo, idadi ya zahanati imeongezeka, na pia idadi ya wahudumu wenye ujuzi imeongezeka, hata utoaji wa meno sasa unafanywa vijijini kama Kanga. Kwa upande wa huduma ya kinga, sasa watoto wengi wanachanjwa kuzuia kifua kikuu, polio, dondakoo, kifaduro na pepo punda. Sasa maisha ya watoto wadogo yanaangaliwa, na kutunzwa vizuri zaidi kuliko pale nyuma. La kufurahisha zaidi, hata mama waja wazito wanaangaliwa vizuri kwa kupatiwa kinga, matibabu na chanjo, hata pia huduma bora za kujifungua. Haya ni maendeleo ya aina yake, natumaini si kwa Kanga peke yake bali kwa Mafia nzima.

***c) Maji***

Nilipokuja mwaka 1965, Mafia.kulikuwa na ukame mkubwa. Kwa mfano, pale Kanga, maji yalikuwa hakuna, na mara nyingine watu walikuwa wakienda kufuata maji mpaka Kirongwe. Hata mimi nilifuata maji Kirongwe, wakati huo. Visima vilikuwa katika hali mbaya sana. Mwaka huu, nimeona visima vingi vizuri vimechimbwa, na wananchi wanapata huduma ya maji kwa urahisi zaidi na maji safi zaidi kuliko pale mwanzo. Kwa hali hii, wananchi wamepunguza kidogo kazi kubwa ya kuchota maji.

**VIZUIZI VYA MAENDELEO HAYA**

Ingawaje hakuna kati yetu hata mmoja hivi sasa anayeweza kusema kuwa hali yetu ni nzuri, na hatuna matatizo ya elimu wala afya, kwa sababu bado kuna matatizo mengi ya vifaa vya mashuleni, waalimu, vitabu, madawati ya kutosha, vifaa vya mahospitali pia madawa, pamoja na hatua hiyo kubwa ya kimaendeleo iliyofikiwa. Ingawaje kuna shule ya sekondari ni jambo zuri, lakini gharama ya kuwasomesha watoto katika shule ile ingali na matatizo, kwa kuwa watoto inawabidi wajitegemee kwa malezi, kwa chakula, na mahitaji mengine. Hii ina maana si watoto wote wenye kupasi kuingia katika shule hii, wanafanikiwa kumaliza masomo yao, kama nilivyokwisha sema

Vivyo hivyo, kuna matatizo katika mwaswala ya afya, katika kutumia kwa mipango: kupatikana kwa dawa za kutosha, na kupatikana dawa za kinga, na wakati mwingine hata kushindwa kutekeleza kabisa kwa mipango yenyewe kwa ukosefu wa fedha. Kwani, wakati mwingine hata mafuta ya taa ya kuwashia jokofu yanakosekana. Hali kadhalika, kama inavyofahamika, watu wengi wanakaa mbali kidogo na vituo vya afya. Kwa hiyo hata wengine hushindwa kutembea kwa miguu kuja mahospitalinl. Vivyo hivyo, hata watumlshl huondoka kila mwisho wa mwezi kwenye hospltali zao kuja wilayani kwa ajili ya kupata mishahara.

Baadhi ya matatizo haya, si rahisi kuyazuia, upatikanaji w a daw a unategemea na serikali, kama vile illvyo kw a w alimu, vitabu, na vifaa vingine. Lakini kama illvyoonyeshw a, na jinsi ilivyofunguliw a shule ya Sekondari, w ananchi pia w anaw eza kusaidia katika nyanja mbalimball, kuongeza juhudi maarifa na hata michango kidogo ili kutatua matatizo kidogo kutokana na uw ezo w ao.

**MATATIZO YA MAENDELEO: MAFIA NA SEHEMU NYINGINE**

Sehemu nyingine mathalan, katika Mafia zimepata maendeleo kidogo tu, kw a maana kuna w engi w amekuw a maskini zaidi kuliko walivyokuw a pale nyuma. Je, hII ni kw a sababu gani? Ili kufahamu hali hii, inatubidi tuangalie mambo tofauti.

- Hali ya uchuml w a dunia
- Hali ya uchumi w a nchi
- Hali ya uchumi w a w ilaya na mkoa
- Hali ya uchumi w a ki3iji na nyumba

Ninajitahidi kulitupia macho kila moja kati ya haya, lakini itabidi ielew eke kw amba vyote hivi vinahusiana kw a karibu mno na kw amba vinaw eza pia kuleta tofauti kw a kila kimoja.

***a) Hali ya uchumu duniani***

Tanzania, na hata klsiw a cha Mafia, ni sehemu ya uchuml w a ulimw engu. Tanzania anaagiza bidhaa kutoka nje, na kusafirisha vitu kama chai, kahaw a, katani, pamba, mafuta, na kadhalika. LakInI uchumi w a dunia kwa sasa ni chini. Hata kw a zile nchi zilizoendelea, uchumi wao upo katika sura mbaya, kw ani kuna hali mbaya ya w atu w engi w asiokuw a na kazi. Ingaw aje, utaratibu ambao uchumi w a dunia umepungua kuendeleza, nchi kama vile USA, Ulaya na Japan, kuw a na njia za kibiashara kuendeleza Asia, Latin Amerika na Afrika. Mpango huu upo kw a sababu mbili zaidi. Kw anza kupanga bei kw a bidhaa ambazo zinasafirishwa na Tanzania, na vile vile kupanga bei ya vitu ambavyo Tanzania inavihitaji kutoka nje, kama vile mafuta, mitambo na vipuli, vitu ambavyo bei zake <u>huongezeka</u> mara kw a mara, wakati mazao ambayo Tanzania inauza <u>hushuka</u> mara kw a mara. Kw a maneno mengine, kununua tractor moja mw aka huu Tanzania ingehitaji gharama mara tatu au nne zaidi ya kiw ango cha nyuma pia, nchi zinazoendelea za magharibi zinaw eza kuziw ekea vikwazo nchi za kusini, na kusababisha usafirishaji kuw a na matatizo.

***b) Hali ya uchui wa Tanzania***

Kutokana na mambo kadhaa muhimu ya kiuchumi, Tanzania inaw eza kulazimika kuingia katika hali ya kukopa madeni makubw a ya pesa hasa kutoka kwenye Mashirika ya Fedha ya Kimataifa yaanI IMF.

Wakati huo, fedha hizo zililazimika kulipwa, kwa riba kubwa. Tanzania si nchi peke yake inayokumbwa na janga kama hili. Nchi zote za Afrika zinakabiliwa na madeni makubwa na mizigo hiyo mara nyingi hukwamisha maendeleo papo hapo. Wakati mwingine inabidi ikubaliane na masharti ya IMF ili kurekebisha hali yake ya uchumi.

- Kuangalia kwa thamani ya fedha ( kunafanya biashara kuwa na gharama zaidi)
- Vivyo hivyo kuanguka kwa mishahara (kunasababishwa na kupanda kwa hali ngumu ya maisha ya wafanyakazi)
- Kutokuwa na bei maalum ya vitu mablimbali (kumesababisha kupanda kwa bei, na hivyo kuathiri gharama za maisha ya watu)
- Kuongezeka kwa riba (kumefanya gharama za mikopo kuwa kubwa)
- Kuharibu utaratibu wa uingizaji wa bidhaa kutoka nje (kumeipunguzia serikali gharama kama vile kutoa fedha kidogo kwa ajili ya huduma za elimu na afya).

***c) Hali ya uchumu wa wilaya***

Nini matokeo ya mambo haya ya kiuchumi katika ngazi za wilaya hasa kwa wilaya yetu ya Mafia?

- Vitu vingi vinapatikana sasa lakini gharama kubwa.
- Mishahara kwa wafanyakazi haikupanda sawa na kupanda kwa maisha.
- Bei za vyakula zimekuwa juu mno.
- Gharama za afya na elimu hazikwenda sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watu na mahitaji yao.

Watu wamekuwa na wajibu wa kulipia gharama za masomo kwa watoto wao, na sasa wanaanza kulazimishwa kulipia gharama za afya. Kwa jumla watu wengi wa Mafia ni wakulima wadogo wadogo wanategemea hasa vitu viwili:

- Chakula kidogo akilimacha kama vile mpunga, muhogo, viazi vitamu.
- Mazao kidogo ya biashara, hasa nazi na korosho.

Kama bei ya mazao kwa wakulima ingeongezeka kulingana na kupanda kwa maisha, basi wasingeona ugumu kupanda kwa bei ya mahitaji yao ya kila siku. Ukweli wa mambo ni kwamba bei za nazi bado hazijaongezeka isipokuwa mkulima anaweza kupata mwaka huu bei nusu kulinganisha na bei ya mwaka jana. Siku hizi wale wanaosafirisha nazi kutoka Mafia kwenda Dar es Salaam, wakisha lipia gharama za usafirishaji, wanabakiwa na kiasi kidogo tu, ambacho hata hicho huwezi kusema kwamba wamepata faida.

Lakini kuna mambo mengine ya hapa ndani yanayozuiaongezeko la uchumi wa Mafia. Baadhi

yake yapo katikangazi za kijiji, na mengine katika ngazi za kaya, nayonitayaoorodhesha hapo baadaye. Kw anza tuangalie haliya w ilaya kw a jumla.

***Njia kuu za uchumi kuwa duni Mafia:***

i) Wilaya ina barabara mbili tu, na hizo zote ziko kw enye hali mabaya sana, na kusababisha usafirishaji w a w atu na bidhaa kuw a na matatizo makubw a. Pia hata vyombo vya kusafirishia huchakaa haraka, hali hii inafanya w asafiri w a ndani w abaki w amekw ama. Papo hapo, usafiri kw enda nje ya Mafia ni tatizo jingine. Watu husafiri kw a mashua ambazo si hatari tu, lakini pia hazina starehe yoyote na kama tunavyoelew a, mashua inasafiri kw a kutegemea upepo na kujaa na kupw a kw a maji.

ii) Njia nyingine ya usafiri ni ya ndege ambayo ni ghali, na hivo haina maalum. Ndege tulizonazo ni ndogo na uw ezo w ake pia ni mdogo. Nimeambiw a kulikuw a na stima ikisafiri kati ya Mafia na Dar es Salaam, lakini sasa haionekani. Kw a hiyo Mafia kw a hali zote haina usafiri maalum kutoka hapa kw enda bara, na matatizo w anayoyapata w atanzania w ote w akiw a hapa kuongezeka kutokana na hali ya Mafia kuw a kisiw a. Kw a hiyo maw asiliano kati ya Mafia na sehemu nyingine za Tanzania, hasa Dar es Salaam, ni magumu na mazito. Hata ndani ya kisiw a, njia kuu ya usafirishaji ni kutembea kw a miguu. Magari mara kw a mara yanaharibika na upatikanaji w a vipuli ni w a matatizo, mgumu, na w a gharama sana. Hata kw a w atumishi w a serikali utendaji w ao w a kazi umekuw a mgumu pia kw a sababu hata kutembelea maeneo yao ya kazi na kukutana na w ananchi w ameshindw a.

iii) Huduma za umeme hakuna isipokuw a Kilindoni, na huduma kubw a ya kazi hutengemea nguvu za jambo ambalo nitachukua muda kuziongelea kidogo. Hata mashine ya kutegemea nguvu ya w atu - baiskeli kw a mfano - zinapatikana kw a uchache na ghali sana. Papo hapo hakuna mashine za kulimia, na kama zipo ni chache mno, na hazitoshelezi kutokana na gharama za uendeshaji; la kustaajabisha hata mashine ndogo ndogo za mikono kama troli, inikokoteni, na inashine za inikono za kusagia hazipatikani.

iv) Vifaa duni vya kuliinia kaina vile jembe 1a mkono, inundu na panga. Kilimo tunachotumia hapa Mafia kinategeinea nguvu za w atu, yaani nguvu kubw a hutuinika inuda inrefu kw a kupata kiasi kidogo kw a inatuinizi inadogo ya inbolea na umw agiliaji, na inategeineo inakubw a bado yapo kw a ajili ya mvua. Tangu utaratibu w a kuw eka kumbukumbu ya kilimo uanzishw e hapa, Mafia bado yaonyesha haijitoshelezi kw a chakula.

v) Gulio la mazao ya biashara yapo mbali na inaeneo ya wananchi. Mara nyingi watu husafirisha inazao yao kwa mfano nazi, kupelekea Dar es Salaam, shughuli ambayo hufanywa na mkulima mwenyewe.

**Ubunifu wa hali ya maisha ya Mafia**

Pamoja na hali ngumu ya maisha, watu wa Mafia inanainudu kuishi hivyo hivyo. Wanaweza kutembea mwendo ndefu kwa ajili ya kuona ndugu na jamaa, kuhudhuria shughuli, kwenda mahakamani, kwenda katika ofisi mbalimbali, na kwenda hospitali ya wilaya na kadhalika. Pia katika misafara kwenda Bara wanatumia ngalawa, mashua na majahazi. Baadhi ya vijiji wamewezа kununua magari, matrekta, na kadhalika. Watu wengine wanafanya kazi kwa bidii, wakitumia nguvu zao kulima mazao ya chakula na biashara. Pia kama nitakavyoendelea kusema hapo baadaye, watu wengine wanafanya kazi kupindukia. Watu wengine pia hujaribu kazi nyingine kwa ajili ·ya kupipatia maisha. Kwa mfano, kwa vijiji vya kaskazini, baadhi ya vijana sasa wanavua kamba ambao wanawapeleka Dar es Salaam na nje, na kupata bei nzuri kuliko samaki. Kwa hiyo, watu wanaweza kubadilika, hawakosi ufumbuzi, wanatafuta shughuli nyingine.

Tunapotafuta vipi tunaweza tukaendelea, ni rahisi kupata majibu kwa ndoto, na kuweza kupata msululu wa vitu, na kusema kwamba kama tukipata vitu hivi, tutafurahi, na kwamba tutakuwa tumepata inaendeleo. Vitu hivyo ni kama:-

- Barabara nzuri,
- Magari ya kutosha kusafirisha watu na mizigo yao.
- Umeme kwa vijiji vyote
- Huduma za simu na posta kwa Mafia nzima

Lakini kaina tunavyojua, vitu vyote hivi haviwezi kupatikana kwa pamoja, au kwa siku moja, vingine kati yake vinahitaji fedha nyingi ambazo si kwa wilaya na hata serikali yenyewe haiwezi ikazipata kwa mara moja. Kwa hiyo, inatubidi tufikiri jinsi tutavyoweza kutumia tulivyonavyo kuweza kupunguza matatizo yetu na kuleta maendeleo na kuboresha hali ya maisha ya watu wetu wilayani? Tunayo ardhi ya kutosha, na tunayo bahari pia. Tunaweza kupata chakula chetu na tuna mazao ya biashara. Mwisho wa hotuba yangu, nitajaribu kutaja mambo ambayo tunaweza kuyafikiria jinsi tunavyoweza kutumia rasilimali tuliyonayo.

Tumejaribu kuzungumzia uchumi wa ulimwengu, uchumi wa taifa, na uchumi wa wilaya. Sasa hebu tuzumgumzie uchumi wa kijiji na kaya.

### *d) Hali ya uchumu kijijini*

Kijiji ni sehemu ndogo ya wilaya ambayo inahitaji shule, kliniki, na utawala, lakini wanakijiji wanaweza wakaungana katika kuendesha miradi kama vile kununua lori au kujenga zahanati. Kwa maana hii vijiji havikai peke yao bila ya kuungana, vijiji vinafaa viungane pamoja na wanavijiji pia wanaungana kijamaa wilaya nzima hata ukanda wa pwani ikiwemo Zanzibar na Pemba.

Papo hapo kuna tofauti baina ya vijiji vya kaskazini, vijiji vimejikusanya pamoja, kila kimoja kimezungukwa na msitu wake. Lakini kusini, kwa upande mwingine, eneo lake lote linepandwa minazi. Kwa hiyo vijiji hivyo kuna nafasi ndogo ya kuliina. Kwa hiyo, kila kijiji kina utaratibu wake maalum wa maisha.

Ni swala la msingi kuona kwamba maendeleo ya kila kijiji hutegemea kijiji kilivyo. Hakuna mtumishi yeyote wa serikali, au mtaalam wa kilimo, uvuvi au ufugaji anayeweza kujua habari za kijiji fulani kupitia wanakijiji wenyewe. Kwa maana hiyo, maendeleo hutegemea ujuzi wa wanavijiji, pamoja na elimu ya wataalamu kutoka nje ya kijiji kile. Maendeleo hupatikana kutoka chini kwenda juu. Lakini utaalamu wa mbinu mpya unapaswa kuletwa kutoka sehemu nyingine na kuenezwa vijijini kwa kupitia mikutano, semina na mafunzo mbalimbali.

### *e) Hali ya uchumi wa kaya*

Kaya ni sehemu muhimu ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, ya uzalishaji na malezi ya watoto, na utunzaji wa watoto na jamii. Kwa maelezo mengine, kaya ni sehemu maalum ambayo kila mtu anaweza akapatiwa matunzo. Watu wote wa kaya wana haki ya kugawana pato la kazi yao. Je, hiyo ndivyo ukweli ulivyo? Si mara nyingi mapato ya watu wote katika kaya moja kulingana. Hebu tuangalie kwa ndani kidogo mambo yanayo husika hapa.

*i) Mgawano wa kazi*

Hapa tunaona wanaume na wanawake wanafanya kazi tofauti. Kwa mfano, wanaume kazi yao ni kufyeka misitu, kuchoma moto na kujenga korti kuzunguka shamba, kuzuia wanyama waharibifu kama vile nguruwe. Kazi ya wanawake kuanzia upandaji, upaliliaji, ulindaji na uvunaji; labda pengine wanaume na wanawake husaidiana kulima viazi na mihogo. Wanaume hufanya kazi zote zinazohusu upandaji wa minazi, na kwa hiyo, wanaume ndio wenye minazi kuliko wanawake.

Hii vilevile kutokana na urithi na desturi tangu huko nyuma na kadhalika. Hali kadhalika wanaume wana muda mwingi wanaweza kufanya shughuli nyingine za kujipatia mapato kama vile uvuvi

wa samaki, kufanya vibarua, au kwenda mijini kutafuta kazi. Kwa wanaume kwa hali hii wana kila sababu ya kupata pesa zaidi, na kuonekana matajiri kuliko wanawake katika kaya, na hata kuwa na mali nyingi kama minazi, mikorosho, ng' ombe, .kuhodhi fedha yote, ndio huwa wanao uwezo wa kuamua jinsi ya kuitumia, kama kununua chakula, chakula gani, kununua nguo, sigara, hata kuoa wake wengine.

Lakini wanawake wana njia chache sana za kujipatia fedha. Wanaweza kuwa na kiasi kidogo cha minazi, lakini hata hivyo shughuli zote za sokoni ni za wanaume. Kwa hiyo, kazi za ziada wanabaki nazo, ili kuwapatia fedha na ukusanyaji wa mikeka mizuri, shughuli ambayo wanawake wa Mafia inawapatia heshima na umaarufu mkubwa. Lakini kutokana na kazi nyingi walizonazo, wanawake wa Mafia humudu kwa mwaka mzima kutengeneza mikeka kati ya sita mpaka minane ambayo huiuza kwa T. Sh. 1,ooo/= tu kwa kila mkeka wakati mchuuzi ambaye ni mwanaume, huuuza mkeka huo kwa Sh. 2,000/= au zaidi huko Dar es Salaam. Ingawa huwa ni pesa chache, wanawake wengi sheria ya mgawanyo wa kazi kati ya mwanamume na mwanamke hapa Mafia ni kama ifuatavyo:

Mwanamume hushughulukia utafutaji wa chakula, mavazi, ada za shule, gharama za kila siku; wakati shughuli za mwanamke ni pamoja na kazi za nyumbani kuanzia kufikicha mpunga, kupepeta, kutwanga, kupika, kwenda maji na kuni, na kuosha vyombo, kuangalia watoto kwa kuwanyonyesha, kuwalisha, na kuwaojesha, pamoja na kusafisha nyumba. Lakini tukitazama ukweli wa mambo, tunaona kwamba wanawake wanashughulikia sana uzalishaji wa chakula, yaani wa kilimo kuliko wanaume. Huwa pia na jukumu la kutafuta pesa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani au nguo, jambo ambalo ni kazi za wanaume, isipokuwa wengi wao hukwepa kwa visingizio vya kutokuwa na fedha, au kuamua kutumia pesa zao kwa vitu vingine. Kwa hiyo tutaona kwamba kazi ya mwanamke ni kama ifuatavyo:

- Kulima mazao ya chakula
- Kufanya kazi za nyumbani, pamoja na kutengeneza chakula, na kulea watoto.
- Kutafuta fedha, kwa mfano kwa kusuka mikeka.

Katika utafiti wangu nilioufanya hivi karibuni, saa za kazi za wanaume na wanawake ni tofauti sana. Wanawake wengi wanafanya kazi kutwa mashambani wakati wa kulima, lakini wanaume si sana kufanya kazi kutwa. Wanawake wanafanya karibu kazi zote za nyumbani, labda wakipata misaada ya watoto wakubwa wakati ambapo hawapo shuleni. Kazi hizo za nyumbani lazima zifanywe kila siku.

*ii) Uzazi*

Baada ya kazi zote hizo, wanawake ndio wanaobeba ujauzito, wanaozaa watoto, wanaonyonyesha kwa miaka miwili. Hapa Tanzania wanawake wanazaa watoto wengi; hesabu ya watoto wastani kwa kila mwanamke ni saba, lakini wanawake wengi wa Mafia wameshika mimba mara kumi au zaidi. Wengi wanaanza kuzaa baada ya kuolewa mapema, kwa umri wa miaka 16, wakaendelea kuwa katika hali ya kuwa waja wazito au kunyonyesha mpaka umri wa miaka arobaini. Mambo haya yana maana gani kwa wanawake, hali yao, na hali ya kaya yao?

- Wanawake wengi wana hali mbaya kiafya, hasa wengi wao wanapata upungufu wa damu.
- Wengi wao wanazaa watoto wadogo mno, ambao wengi wanakufa mapema.
- Wanawake ambao ni wajawazito, au wamezaa hivi karibu, hawawezi kulima kama kawaida, kwa hiyo kila wakati ambapo mwanamke anazaa wakati wa kulima, kaya inapata mavuno machache. Kwa hiyo, lazima watu wake walime chakula zaidi. Kwa maneno mengine, kiwango cha malishaji, hasa cha mazao ya chakula, kinaathiriwa na swala la uzazi. Uzazi unaathiriwa pia na swali la ulishiaji. Mwanamke mja mzito akifanya kazi mno anaweza kuharibu mimba yake, au kupata mtoto dhaifu ambaye hatimaye hufa.

*iii) Chakula*

Sasa natuingie katika swala lingine linalohusu kaya sehemu ambaye chakula hugawanywa. Katika utafiti wangu, nimeweza kugundua kwamba wanawake wanapokula chakula, wanawapa chakula kingi na kizuri wanaume kuliko wenyewe. Hivi kwa nini? Wanawake wanasema kama ifuatavyo:-

- Wanaume hukasirika sana kama hawakupewa chakula kizuri na kingi.
- Wanaume huhitaji chakula kingi zaidi kuliko wanawake kwa sababu kutokana na kazi wazifanyazo ni muhimu zaidi.
- Wanawake wanoa uwezo wa kustahimili njaa zaidi kuliko wanaume hii ni hali ya maumbile

Lakini hali ya chakula ambacho mwanadamu anahitaji, hutegemea mambo mengi kama umri, uzito na urefu, kazi wazifanyazo (wale wanaofanya kazi za nguvu hula zaidi) na hali yao (mwanamke mja mzito au anayenyonyesha, huhitaji chakula zaidi kuliko mwanamke wa kawaida).

Sehemu kubwa ya chakula katika nyumba hapa Mafia hununuliwa kwa sababu nyumba chache hupata chakula wanachohitaji kwa mwaka. Kwa hiyo hununua sana unga wa dona. Zaidi ya

hayo, hununua kitoweo kama maharage au samaki, na mara chache kuku au nyama. Hii ni njia muhimu ya kujipatia protini nani ambayo ni muhimu hasa kwa ukuwaji wa wototo, kuwasaidia kujenga miili yao na akili zao.

Moja kati ya matatizo tunayoona hapa na sehemu nyingine ni kwamba kila serikali au mtaalamu anapozungumzia swala la chakula bora, hasa kwa watoto, husema wanawake wanahitaji kuelemishwa. Lakini si hivyo, mara nyingi wanawake wanafahamu juu ya kinachohitajika lakini kinacho kosekana ni nguvu ya kuamua kipi kinunuliwe au uwezo wa kifedha. Wanaume, kwa upande mwingine, wanaweza wakawa na yote haya; uwezo wa kuamua nini anunue, na fedha, lakini hukosa ujuzi juu ya chakula kipi ni muhimu kwa watoto wake na mwanamke mja mzito au anayenyonyesha. Vile vile, mwanamume anaweza asitambue kiasi gani cha kazi mwanamke anafanya, na kutolipa swala hili uzito unaostahili, au wanaweza hata kupuuzia kazi wanazozifanya wanawake huwa hazina umuhimu au si nzito kulingana na kazi wanazozifanya wao. Kwa hiyo, kazi ya wanawake haionekani umuhimu wake na kukosa kuthaminiwa au kwa kifedha hata kwa chakula.

Je, sasa tufanye nini ili kusaidia kuinua hali hii katika kila nyumba?

**Mabadiliko yanyohitajika nyumbani**

Kwanza kuwapunguzia kazi wanawake, hasa waja wazito na wanaonyonyesha.

Je, kwa kufanyaje?

- Msaada mkubwa unahitajika kwa watu waliobaki katika nyumba, kama vile watoto wakubwa na wanaume kuwasaidia wanawake. Kwani hakuna ubaya wowote utakaotokea kwa mwanamume katika kuisadia kazi za nyumbani. Lakini ni vibaya sana mtu mwingine kukaa tu akiwatazama wenzio wanapata taabu na kuumia kwa kazi nzita za kila siku, ambazo kuwafaidia wote.
- Njia nyingine ya kugawana rasilimali ya ·nyumba kwa usawa kuanzia chakula na hata fedha. Si jambo la kushangaza kwa watu wa Mafia kwamba wanaume ndio mara nyingi hula mahotelini na mitaani kuliko wanavyofanya wanawake. Nadhani swala kubwa hapa ni uwezo wa kifedha.
- La tatu, kuongeza kiwango cha chakula na lishe katika nyumba zetu, sababu tumekwishaona kwamba wanawake na watoto hawana sehemu nyingine ya kupata vitu hivi.
- La nne, ni kufikiria kuwa pamoja mwanamke na mwaname katika nyumba jinsi gani wataweza kupata pato zaidi la fedha kwa maisha yao, ili waweze hata kutoa matunzo

ya ziada kwa watoto wao kama zile kuweza kulipia ada za shule na uanzishaji wa miradi mingine midogo midogo kwa maisha yao.

- La tana njia nyingine ni kupunguza uzazi wa mara kwa mara, ambao unampa mwanamke nafasi ya kupumzika kati ya mtoto na mtoto; swala hili ni muhimu sana kwa afya zao. Zaidi ya yote ni muhimu pia kwa mtoto kupata kunyonya kipindi cha miaka miwili na kumpatia afya bora. Nadhani tunakubaliana kuwa hata mafundisho ya dini yanatueleza hivyo. Kwa hiyo ni vizuri akina mama wachukue uja uzito baada ya miaka miwili au zaidi.
- La sita si vyema watoto wakiwa bado wadogo kuzaa, sababu watakuwa hajakomaa kiakili na kimwili. Vile vile, si vizuri kabisa kwa akina mama wenye umri zaidi ya miaka 35 kuzaa sababu watakuwa wamechoka na kuweza kusababisha kushindwa kutunza mtoto, na pia kuweza kusababisha kuwazaa watoto tofauti tahira au wasiojiweza. Hali hii ni hasara kwa ulimwengu, taifa, mkoa, wilaya, kijiji, mtaa, hadi nyumba.

Katika utafiti wangu, nimepata kusikia kutoka kwa wanawake wengi wa hapa Mafia wakisema kuwa wangependa zaidi kutumia uzazi wa mpangilio ili wapate kupumzika, lakini waume zao hawapendi mpango huu, na wengi hawataki hata kusikia hatimaye sisi mwenyewe kama wazazi kwa hiyo, uamuzi mkubwa wa utaratibu gani nyumba au kaya ichukue katika maswali ya uzazi, yanamtegemea zaidi mwanamume. Kwani kwa wao watoto ni utajiri , na kwamba utajiri wa mtu maskini ni watoto. Watu wote duniani wanakubaliana na ukweli huo, lakini kuna utaratibu wake, na tunavyosema hivyo, tunashawishika kwamba kuwa na watoto wengi pamoja ni mzigo tunaokubebesha.

**MWISHO ( SHINIKIZO)**

**Mapendekezo:**

Mapema katika hotuba yangu nimesema tunapozungumzia swala la maendeleo yatupasa tujiulize maswali yafuatayo:

Kwanza , nini tunataka?

Pili, ni vipi vitakavyo tusaidia kupata mahitaji yetu?

Tatu, nini matokeo kutokana na maendeleo hayo? Ni maendeleo kwa watu wote au ni maendeleo kwa watu wachache? Pia nilisema Mafia inayo rasilimali:

- Watu wake na elimu yao
- Utaratibu walionao; ardhi nzuri; na bahari.

Kutokana na babadiliko mafupi, tunaweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

***I. Kuzidisha uzalishaji wa chakula.***

Kama watu wengi wataalam sana, wataweza kujipatia chakula cha kutosha, wataweza kutumia baadhi ya fedha wanazozipata kununua vitu vingine
kama nguo nzuri, watasomesha watoto wao vizuri, na watanunua vitu vingine kama vile redio na baiskeli. Je, tutayapataje haya?

- Tutayapata haya kwa kuwashawishi wakulima kulima zaidi na kupanua mashamba ya chakula
- Kumfundisha kila mkulima, wanawake kwa wanaume, kulima kwa kutumia njia bora za kilimo.
- Kumsaidia kila mkulima kupata vifaa bora vya kulimia na kuvuna.
- Kumshauri mkulima jinsi ya kuhifadhi chakula chake.
- Ni bora ieleweke kuwa kuvuna vizuri maana yake ni kupata chakula cha kutosha na kukihifadhi kwa matumizi ya baadaye.
- Njia nyingine ya kuongeza pato la mkulima ni kuongeza ulimaji wa mboga za aina mbalimbali kama vile mchicha, nyanya, bamia, matango, matikiti, maboga, fivi, kunde,
- na kadhalika.

***2. Utuimiaji wa mbinu bora na za kisasa***

Utumiaji wa njia rahisi za kilimo kwa kutumia rasilimali tulizonazo unaweza ukafanya kilimo chetu kiwe na matatizo makubwa, kwa mfano kupanda mazao kwa mistari au kwa hatua zinazopendekezwa na kilimo bora zinaweza kumzidishia mkulima mapato. Nadhani mnakubaliana na mimi kwamba si kila mtu kati yetu anaweza kununua trekta wa ajili ya kulimia, na wala siyo uwezo wa serikali yetu. Kwa nini tupoteze wakati wetu kufikiria upatikanaji wa matrekta ya kutosha kwa ajili ya kulimia wakati tunaweza tukazalisha vizuri na kwa urahisi kwa kutumia ujuzi na vifaa tulivyonavyo? Kwa hiyo, si bora wataalam wetu wa kilimo watuelezee zaidi mbinu za kilimo rahisi ambacho kila mkulima wetu anaweza kazitumia?

***3. Ufugaji bora***

Ufugaji bora wa ng'ombe maana yake ni kupata nyama kwa wingi na maziwa kwa wingi kwa ajili ya lishe, na vilevile kuweza kupata mifugo yenye uwezo wa kutusaidia katika kilimo na kubebea mizigo yetu, pia na upatikanaji wa mboleo wa kutosha. Si vibaya hapa tulipo tukifikiria upatikanaji wa biogas kwa ajili ya kujipatia umeme kwa urahisi kuliko kufikiria umeme kama huu tulionao hapa Kilindoni ambao hutegemea mafuta ghali.

Ni vizuri vile vile tuwahimize wakulima wetu na wananchi kwa ujumla ufugaji wa wanyama wanaostawi vizuri hapa kwa gharama nafuu kama vile kuku, bata, punda na mbuzi: kuku na bata kwa ajili ya mayai na fedha, mbuzi kwa ajili ya maziwa na nyama, punda kwa ajili ya kubebea mizigo.

***4. Uendelezaji wa kilimo cha biashara***

Ndugu zangu nionavyo mimi, ninyi watu wa Mafia mna bahati kubwa kuwa na ardhi nzuri kwa maisha yenu kama mngeitumia vizuri kwa ulimaji wa mazao ya biashara, badala ya minazi na mikorosho peke ·yake mngeweza kupata fedha nyingi. Sehemu mlizopanda minazi na mikorosho bado zinatoa nafasi kwa kupanda mazao mengine ya muda mfupi ya biashara kama vile kokoa, pilipili, mapapai, ndizi, machungwa, na mboga mboga. Je, kwa nini hatufanyi hivi? kuna sheria ·yeyote ndogo iliyowekwa na serikali inayowazuia msifanye hivyo?

***5. Soko lingine la minazi***

Hivi sasa, soko letu la nazi la Dar es Salaam limezidiwa na hivyo kusababisha nazi zetu zikose bei nzuri. Yatubudi hivi sasa tutafute njia zingine. Kwa mfano nimesikia kwamba Mafia Coconuts Limited (MCL) sasa hivi ina mpango mpya wa kuboresha mashamba yake na kusinjika upatikanaji wa mazao ya minazi kwama vile mafuta , sumba, vifuu, na unja wa vifuu, na kuuza nje. MCTh pia ingeweza labda kununua nazi kutoka kwa wakulima wengine, na kusaidia kwa upatikanaji wa soko kwa urahisi kuliko ulivyo sasa.

***6. Njia zingine za kupatia mapato***

a) Bahari nzuri tuliyonayo tungeweza kuitumia kuanzisha mashamba ya mwani kuliko kuishia na kuvua samaki peke yake. Hali kadhalika hata uvuvi wenyewe ungebalidisha kidogo kwa kuwasaidia wavuvi wetu kupata msaada au mikopo ya kuwapatia vifaa bora na vya kisasa vya uvuvi. Kwani kufanya hivyo kutasaidia upatikanaji wa samaki wengi na wazuri na kwa hali hiyo wavuvi wetu wapate fedha na kuweza kumudu maisha yao vema zaidi. Ni vizuri tunapozungumza ugumu wa maisha tuonyeshe jinsi gani tunajitahidi kukabiliana nayo sisi wenyewe kwa njia nafuu tulizonazo.

b) Ufugaji wa nyuki. Inavyoonekana, hali ya hewa ya Mafia inaruhusu ufugaji wa nyuki. Je, isingekuwa bora tukaanzisha mashamba ya nyuki kwa ajili ya asali na nta? kwa mfano pale Kanga chupa moja ya asali inauzwa kati ya sh.400/= mpaka 700/=. Je, hii isingesaidia?

***7. Uanzishaji wa ushirika wa watenegengezaji wa mikeka vijijini***

Kisiwa cha Mafia kina bahati ya kuwa na wasukaji wazuri wa mikeka, lakini wanakosa namna ya kuendeleza kazi hiyo na kuitegemea. Hivi sasa wasukaji wengi vijijini wanakabiliwa na matatizo mawili: kwanza upatikanaji wa rangi za mikeka, na pili, soko la mikeka. Kwa nini ufundi huu tusingetumia kuwapatia wananchi wetu pato kwa maisha yao? Kuna haja gani kuanzisha miradi mikubwa na migeni wakati tunaiacha mizuri na ya gharama nafuu inayoweza kutupatia pato kubwa kwa wananchi wetu? Ingefaa tutupie macho vitu kama hivi ili kuinua hali ya maisha yetu kwa urahisi na haraka zaidi, natubidi tutilie mkazo mambo muhimu mawili: kuboresha njia ya usafirishaji ndani ya Mafia na nje ya Mafia. Tunahitaji barabara nzuri, na usafari wa stima wakati wote. Nimepata habari karibuni kwamba barabara zetu zinatengenezwa. Ukweli ni kwamba kama hali za barabara zote zitakuwa nzuri naamini itaamsha maendeleo kwa wilaya nzima.

Haya ni mapendekezo yangu tu - mengine yanawezekana, mengine hayawezekani, kama tungeongeza uzalishaji wa kila mtu, tungeweza kuinua hali ya maisha na hali ya kinga ya mili yetu kwa magonjwa. Kufanya hivyo , ndio kuishi vizuri. Na kama tungeweza kuinua pato letu la kila siku, tungewawezasha watu wetu kuwa na vitu vingi. Kwa ufupi, tungemfanya kila mtu kuwa na maisha bora.

Mwisho zaidi, nimefurahia sana na safari ya mwaka huu kwani nimekuja Mafia mara tatu bila ya kupata bahati ya kukaribishwa nizungumze chochote wilayani, lakini mwaka huu kutokana na kuanzishwa kwa Chama Cha Maendeleo ya Mafia (Chamama) kumenifanya mimi niwe hapa leo na kuweza kuongea na nyi hapa. Na vili vile nimefurahi sana kuona kwamba NGO kama Chamama imeanzishwa hapa Mafia. Natumaini mtanivumilia na kunisamehe kwa yote yale ambayo labda hayakuwafurahisha. Yawezekana yote hayo ni kutokana na mchanjo wangu mdogo wa lugha ya Kiswahili. Nawashukuru wote kwa kuja kunisikiliza.

ASANTENI SANA, NA KWAKERINI